Swali: Muujiza wa kwanza wa Bwana YESU ulikuwa ni upi?

---

Jibu: Mwujiza wa kwanza wa Bwana YESU ni ule wa Kana ya Galilaya, ambapo aligeuza maji kuwa Divai.

> *Yohana 2:1 “Na siku ya tatu palikuwa na arusi huko Kana, mji wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwapo.*
>
> *2 Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake.*
>
> *3 Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akamwambia, Hawana divai.*
>
> *4 Yesu akamwambia, Mama, tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadia.*
>
> *5 Mamaye akawaambia watumishi, Lo lote atakalowaambia, fanyeni.*
>
> *6 Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe, nayo*

> *yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha, kila moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu.*
>
> *7 Yesu akawaambia, Jalizeni mabalasi maji. Nao wakayajaliza hata juu.*
>
> *8 Akawaambia, Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza. Wakapeleka.*
>
> *9 Naye mkuu wa meza alipoyaonja yale maji yaliyopata kuwa divai, (wala asijue ilikotoka, lakini watumishi walijua, wale walioyateka yale maji), yule mkuu wa meza alimwita bwana arusi,*
>
> *10 akamwambia, Kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa.*
>
> *11 MWANZO HUO WA ISHARA YESU ALIUFANYA HUKO KANA YA GALILAYA, akaudhihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamwamini".*

*Mstari huo wa 11* unatudhihirishia wazi kuwa hiyo ndio iliyokuwa

ishara ya kwanza kufanywa na BWANA YESU mbele ya wanafunzi wake.

Sasa kujua kwa mapana ujumbe uliopo nyuma ya muujiza wa kwanza wa Bwana YESU wa Kana ya Galilaya fungua hapa >>Kwanini Bwana YESU ageuze maji kuwa Divai? Na ni ujumbe gani tunapata?

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx1

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

NI NINI BWANA ANATAKA KUTOKA KATIKA MUUJIZA ALIOKUFANYIA?

JE UMEJIANDAA KUTIMIZA UNABII UPI?

Kumaka ni nini katika biblia? (Mathayo 8:27)

SIRI KUU NNE (4), UNAZOPASWA UZIFAHAMU NDANI YA KRISTO.

UFUNUO: Mlango wa 3 part 3

MIMI NIKO AMBAYE NIKO

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp